

**MAKUBALIANO YA KUPANGISHA ENEO KWA MATUMIZI OFISI YA  
BIASHARA**

**MAKUBALIANO HAYA YAMEFANYIKA** leo tarehe 31..... Mwezi 03.....2023

**BAINA YA**

**ALI ABDI ALI** mkazi wa Unga Limited, jijini Arusha, Tanzania ambapo hapa anatambulika kama "Mpangishaji" kwa upande mmoja.

**NA**

**YUSSUF ABDIRAHAMAN YUSSUF** mwenye anuani ya Ofisi S.L.P 62, Arusha, Tanzania ambapo hapa anatambulika kama "Mpangaji" kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** Mpangishaji ni mmiliki halali wa Eneo lililopo kwenye plot nambari 11 ndani ya block 11 jengo namba 11 eneo la Unga Limited Wilaya ya Arusha jijini Arusha, Tanzania.

**KWA KUWA** Mpangishaji kwa hiari yake mwenyewe amekubali kupangisha eneo tajwa hapo juu kwa matumizi ya kuegesha magari kwa ndugu **YUSSUF ABDIRAHAMAN YUSSUF** kwa makubaliano yao kama yanavyoonekana hapo chini.

**SASA PANDE ZOTE MBILI WAMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO: -**

1. Kwamba Mpangishaji amepangisha eneo na Mpangaji amekubali kupanga katika eneo hilo kwa matumizi tajwa hapo juu.
2. Kwamba mkataba huu wa kupanga utakuwa ni wa Miaka Mitano na utaanza tarehe 31/03/2023 hadi tarehe 31/03/2028.
3. Kwamba Kodi kwa mwezi itakuwa ni kiasi cha Shilingi Milioni Moja (TSh. 1,000,000/=) tu.
4. Kwamba Mpangaji hataruhusiwa kufanya marekebisho ya eneo tajwa bila idhini ya Mpangishaji.
5. Kwamba Mpangaji hatakuwa na mamlaka ya kumpangisha mtu mwingine katika kipindi hicho cha Miaka Mitano na pia Mpangishaji hatakuwa na mamlaka ya kumbughudhi Mpangaji.
6. Kwamba Mpangaji akitaka kuongeza mkataba atamtaarifu Mpangishaji mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha. Mpangishaji atakuwa na hiari ya kukubali au kukataa kuongeza mkataba huo.

**MAKUBALINO HAYA** Yametiwa saini leo tarehe 31 Mwezi 03 2023 mbele ya mashaidi kama ifuatavyo:-

**UMETIWA SAINI** na **ALI ABDI ALI**

ambaye amefahamishwa Mimi binafsi

na .....

leo tarehe 31 mwezi 03 2023

*Ali*

MPANGISHAJI

**UMETIWA SAINI** na **YUSSUF ABDIRAHAMAN YUSSUF**

Ninayemfahamu/ ambaye amefahamishwa kwangu na

..... Ninayemfahamu leo

tarehe 31 mwezi 03 2023.

*Yussuf*

MPANGAJI

**MBELE YANGU:**

JINA: NENILE JOSEPHINE DAVID

SAINI: *David*

ANUANI: 3238 DAR-ES-SALAAM

WADHIFA: WAKILI.

